

2: Transcript- Chovya Chovya

- Baba Chaurembo: Habari mama?
- Mama Chaurembo: Nzuri tuu baba, leo umewahi kurudi, karibu.
- Baba Chaurembo: Asante mama, yaani leo kule kazini nimepata kifuta jasho.
- Mama Chaurembo: Hongera sana baba!
- Baba Chaurembo: Asante sana, sasa mimi nilikuwa nafikiria hapa nyumbani tuna shida moja, unajua shida yenyewe ni ipi? Kabati la vyombo.
- Mama Chaurembo: Yaani kweli kama ulijua! maana hata mimi nilikuwa nafikiria hivyo hivyo, hatuna mahali pa kuviweka vyombo hata vingine vimeshavunjika.
- Baba Chaurembo: Chukua hizi hela uziweke (anahesabu, 12, 34, 56) naomba hii hela usiiguse hiyo nyingine niwekee pembedi tutaonana baadaye.
- Mama Chaurembo: Unaenda wapi sasa?
- Baba Chaurembo: Naenda kwa jirani kuzunguka kidogo.
- Mama Chaurembo: Basi usichelewe.
- Baba Chaurembo: Sitachelewa mke wangu.
- Muuza nguo: Wakina mama! jamani kuna mashati, vitenge, wale wa nguo tunapita jamani!
- Mama Chaurembo: Wewe njoo,
- Muuza nguo: Yaani leo nimekuletea vitu freshi,

- Mama Chaurembo: mashati mazuri kabisa.
- Muuza nguo: Mpende mumeo, vitu vizuri
- Mama Chaurembo: Hebu lete nione, ndio shilingi ngapi?
- Muuza nguo: Vitenge shilingi elfu kumi!
- Mama Chaurembo: Elfu kumi bei ghali!
- Muuza nguo: Tena hapo nimekupunguzia, tena hiyo saizi yako.
- Mama Chaurembo: Tena hicho kitenge usikiachie kabisa!
- Mama Chaurembo: Haya nipe hiyo bwana.
- Muuza nguo: Yaani hiyo ni nzuri kabisa tena na mzee akivaa shati lake mnatoka kabisa.
- Mama Chaurembo: Wewe si unavutia tuu biashara?
- Muuza nguo: Wewe nipe hela bwana!
- Mama Chaurembo: Mama mbona hutoki?
- Mama Chaurembo: Siunajua hela zipo mbali, Haya chukua shoga.
- Muuza nguo: Haya asante.
- Mama Chaurembo: Nitakuletea magauni ya watoto.
- Mama Chaurembo: Haya!
- Muuza viatu: Baada ya dakika tano.
- Mama Chaurembo: Pata viatu dada, habari za leo dada?
- Muuza viatu: Salama tuu umeshindaje?
- Mama Chaurembo: Nzuri tuu.
- Mama Chaurembo: Naona leo upo kwenye biashara.

- Muuza viatu: Ndiyo nipo kwenye biashara dada yangu.
- Mama Chaurembo: Viatu bei gani?
- Muuza viatu: Nipe elfu saba tuu dada yangu.
- Mama Chaurembo: Haya subiri!
Zile hela nilizozichukua kununulia nguo nachukua tena , kununulia viatu najua kabati haliji leo ngoja tuu nikanunue viatu.
Njoo chukua hela basi.
- Muuza viatu: Haya dada yangu asante.
Baadaya ya siku mbili.
- Baba Chaurembo: Sasa mke wangu, lile kabati kule kwa fundi limeshaisha kwahiyio naomba zile hela nilizokupa kipindi kile ili nikitoka kazini nije nalo.
- Mama Chaurembo: Baba Chaurembo, yaani tayari mara hii?
- Baba Chaurembo: Ndiyo yule fundi ni mzuri sana anatengeneza haraka sana, yaani hatu wewe ukilionia utafurahi.
- Mama Chaurembo: Haya sogea.
- Baba Chaurembo: Haya.
- Mama Chaurembo, pesa nilizokupa zimekwenda wapi?
- Mama Chaurembo: Samahani mume wangu, sikujua fundi atatengeneza kabati kwa haraka hivyo. Nilikuwa nategemea kupata hela zangu

za mchezo, umefanya nini sasa?

Vocabulary

Kifuta jasho- Bonus

Shoga – “girl friend”